**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO**

**SHULE YA SEKONDARI SOKOINE MEMORIAL**

**Namba za Simu…………………..**

**Mkuu wa Shule 0658-046693**

**0755-046693**

**Makamu Mkuu wa Shule 0718-837539**

**0787-436573**

**Matron/Patron 0712-801553**

**Shule ya Sekondari Sokoine Memorial**
**S.L.P 6568, Morogoro**

**Tarehe 06 Juni, 2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI SOKOINE MEMORIAL ILIYOPO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO, MKOA WA MOROGORO, MWAKA 2023/2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023/2024 na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari Sokoine Memorial ipo umbali wa Kilometa 38 Kaskazini/Kusini/Mashariki/Magharibi mwa Mji wa Morogoro. Usafiri wa basi

kutoka mjini upo. Unapatikana nje ya katika kituo cha mabasi Msamvu katika sheli ya ATN panda gari zinazokwenda Dakawa au Dumila au Gairo, Nauli ni Shilingi 3000/=.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 1**3/08/2023** kwa kidato cha tano TU hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 1**3/08/2023**.Masomo yataanza tarehe 14/08/2023.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni Suruali rangi ya ugoro (Brown).Iwe na marinda mawili mbele, pindo la chini ligeukie juu (Turn up) isiyobana (modo) ndefu mpaka kwenye vifundo vya miguu Mwanafunzi anatakiwa awe na Jozi mbili za Suruali.
ii. Mashati mawili meupe ya Mikono mifupi, Mshati yawe na nembo ya shule. Aina ya kitambaa ni Tomato.
iii. Sare ya Michezo ni Track suit rangi ya bluu iliyokolea na raba (Jozi Moja inatosha);
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta Moja rangi ya ugoro (Brown) shingo iwe ni ya v, pia liwe na Mikono mirefu.
viii. Nguo za kushindia Fulana Moja rangi ya Dhahabu(Gold) Shingo iwe ya duara (round), iwe ya Mikono mifupi, iwe na nembo ya shule. Suruali moja ya kitambaa rangi nyeusi, Sio modo iwe ndefu
ix. Tisheti (T-shirt) maalumu ya shule rangi ya kijivu, (Aina ya mshono iwe yenye kola, Mikono mifupi - maarufu 'Form Six'). Iwe na nembo ya shule

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 8 'Counter Book' Quire 3 au 4 ;
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi za photocopy Bunda Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwa*);

**VITABU VYA KIADA NA ZIADA**

| GENERAL STUDIES | HISTORY | GEOGRAPHY | ENGLISH LANGUAGE | ECONOMICS | ADVANCED MATHEMATICS |
|---|---|---|---|---|---|
| Understanding Advanced level General Studies by Bigiwamungu & Sospeter | 1. Advanced Level History for Form 5&6 by Oxford<br><br>2. Advanced Level History Paper 1&2 by Z.Kamili<br><br>3. Essential for Advanced Level History Paper 2 By Salehe Yasini<br><br>4. Mastering of History Paper 1, By Kassim Kato<br><br>5. Mastering of History Paper 2, By Kassim Kato | **1.** Practical Geography for advanced sec. schools form 5&6 by TIE<br><br>2. Physical Geography for advanced sec. schools form 5&6 by TIE<br><br>3. Human Geography for advanced sec. schools form 5&6 by TIE<br><br>4. A Comprehensive Approach to Physical Geography By D.T. Msabila | 1. Advanced Level Literature by N. Asheli<br><br>2. Contemporary English for Advanced level by Francis Mnyawi<br><br>3. New advanced Level English by Charles | **1.** Micro economics for Advanced Sec. Schools Form Five By TIE<br><br>**2.** Micro economics for Advanced Sec. Schools Form Six By TIE<br><br>**3.** Essentials For A-Level Economics Paper 1 Form Five By Ambros Odhiambo<br>**4.** Essentials For A-Level Economics Paper 2 Form Six By Ambros Odhiambo | 1. Advanced Mathematics for Form 5 By TIE<br><br>2. Advanced Mathematics for Form 6 By TIE<br><br>3. Advanced Mathematics for Advanced Sec. Schools Form 5 By Septine I. Sillem.<br><br>4. Advanced Mathematics for Advanced Sec. Schools Form 6 By Septine I. Sillem |

iv. Scientific Calculator;

v. Godoro futi mbili na nusu kwa sita lenye foronya ngumu.

vi. Mashuka rangi ya bluu Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua kimoja cha rangi ya bluu.

vii. Nguo za ndani za kutosha, ndala, kitana

viii. Vyombo vya chakula (sahani , bakuli, kijiko na kikombe); Vyombo vya plastic haviruhusiwi.

ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

x. Buti kwa ajili ya kujizuia na tope wakati wa mvua

xi. Kwanja 1, jembe 1, panga 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

xii. Dawa ya kusafishia Tiles/Vyoo. Lita Moja. Jina la Dawa; ARO au NEW TRILIONNAIRE PURE CLEANER

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Michango hii ilipwe kwenye AKAUNTI ya shule NMB 22710016099. Sokoine Memorial High School**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| JUMLA | | **70,000/=** |

**Kumbuka kuleta Risiti halisi (Pay slip)**

**b) Michango hii utakuja Lipa shuleni**

| **1** | **Nembo** | 5000/= |
|---|---|---|
| 2 | Kitambulisho Cha shule | 5000/= |
| **JUMLA** | | **10,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**


i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** 

**Jina la Mkuu wa Shule: Gosbert Rweyemamu Rwegasira**

**Muhuri wa Mkuu wa Shule** 

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0755-046693/0658-046693**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0718-837539/0787-436573**
- **Mwandamizi Taaluma 0652-385992**
- **Mwandamizi Malezi 0755-030375/0712-801553**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI SOKOINE MEMORIAL**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA**

| PICHA YA MWANAFUNZI |
|---|

**A: TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**:

JINA LA MWANAFUNZI________________________________________
TAREHE YA KUZALIWA_______________________________________
MAHALI ALIPOZALIWA (MKOA/WILAYA)___________________________________
MAHALI ANAPOISHI (KATA/MTAA)________________________________
URAIA___________________________
SHULE YA SEKONDARI ALIYOTOKA___________________________
NAMBA YA MTIHANI__________________________________________

**B: TAARIFA YA MZAZI:**

JINA LA MZAZI/MLEZI_________________________________________
KAZI YA MZAZI/MLEZI_______________________________________
ANUANI YA MZAZI/MLEZI______________________________________
SIMU YA MZAZI/MLEZI (tafadhali andika namba za simu zinazotumika na mhusika kama ni mama au baba nk.

______________________________________________________________________________

**C: KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA (MWANAFUNZI)**

Mimi____________________________________Kidato cha________mwaka________Nimesoma na kuyaelewa yote. Kwa hiyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba Nimepokea maagizo au maelekezo bila kulazimishwa kuyazingatia.

Tarehe______________________ Sahihi________________________

**D: KUKUBALI SHERIA ZA SHULE :( MWANAFUNZI)**

Mimi____________________________________nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na naahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria za shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu na viongozi wote wa shule, nikikiuka sheria hizohatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria zilizopo.

Tarehe______________________ Sahihi_________________________

**E: MZAZI/MLEZI – (Ajaze sehemu hii)**

(i) Mimi_______________________________Mzazi/Mlezi wake nathibitisha kuwa Mwanangu (jina la mtoto)__________________________________ameelewa maagizo na ninapenda ifahamike kuwa dini ya mwanangu ni__________________________dhehebu lake ni___________________________

(ii) Ninaruhusu/Siruhusu (kata isiyohusika) mwanangu kushiriki katika Makongamano au Warsha za kidini nje ya shule zinazofanyika nje ya Mkoa wa Morogoro pasipo na Mwalimu wa shule hii.

(iii) Ninaruhusu/Siruhusu (kata isiyohusika) wakati wa likizo fupi (mid-terms) atoke.

Shuleni na kwenda kwa__________________________wa (mahali)_________________________

Uhusiano wake na Mwananguni____________________Namba yake ya simu ni________________.

(iv) Aidha mimi________________________ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi nimesoma/nimesomewa sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi (jina la mwanafunzi)___________________________nakuahidi kutimiza wajibu wangu nikiwa Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa kumshauri ipasavyo pamoja na kumtimizia mahitaji yake ya shule.

**JINA LA MZAZI/MLEZI__________________________SAHIHI YA MZAZI/MLEZI_____________**

**TAREHE___________________________**

**F. SEHEMU YA NDUGU WA KARIBU**

Ndugu wa karibu wanaoruhusi wa kumtembelea mwanafunzi: BABA MAMA

| | JINA | UHUSIANO |
|---|---|---|
| 1 | _________________________ | _______________________ |
| 2 | _________________________ | ______________________ |
| 3 | _________________________ | _______________________ |
| 4 | _________________________ | _______________________ |

MLEZI -01 MLEZI-02

***MUHIMU***: **kutembelea mwanafunzi ni jumamosi ya mwisho wa kila mwezi**, tofauti na hapo hutopokelewa. Pia mwanao ataruhusiwa kwenda likizo fupi kwa mtu au mahali ulipoelekeza wewe hatutapokea mabadiliko kulingana na maelekezo ya mwanafunzi

**G. KIKAO CHA WAZAZI**

Kitafanyika mara moja kwa mwaka wa masomo 2023/2024.Wazazi/walezi mtaarifiwa siku na tarehe ya kikao hicho.

**Masharti mahususi**:

1. Ni lazima mzazi/Mlezi kuhudhuria kikao

2.Udhuru wowote hautakubalika

3.Kwa mzazi/mlezi asiyefika siku ya kikao atalipa faini ya shilingi elfu hamsini (50,000) Vinginevyo mwanafunzi hatapokelewa na atalazimika kurudi alikotoka

**H. SEHEMU YA MZAZI KUKIRI KUHUDHURIA KIKAO CHA WAZAZI**

Mimi____________________________mzazi wa __________________________wa kidato cha_______

Nitahudhuria kikao cha wazazi bila kukosa hapo shuleni kwa tarehe itakayopangwa

Sahihi_______________________Tarehe_____________________

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A**

The Headmaster,
Sokoine Memorial Sec. School,
P.O. Box 6568,
**Morogoro**.

**To the Medical officer,**

__________________________
__________________________
__________________________

________________________________________ (Name of student in full) Please examine the above named student as to his physical and mental fitness for a full-time student. The examination should include the following categories (a-d)

(a) (i) Eyesight (ii) Hearing (iii) Speech (iv) Venereal diseases (v) Limbs
(vi) Leprosy (vii) Epilepsy
(b) Neurosis
(c) Other serious diseases eg. Asthma, Tb etc

Name of head of school: **Gosbert R. Rwegasira:** Signature [signature] Date: 06 Juni. 2023

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer) I have examined the above student and consider that he is fit/unfit for full time studies.

(i) Eyesight____________________________________
(ii) Hearing____________________________________
(iii) Speech____________________________________
(iv) Limbs____________________________________
(v) Venereal diseases____________________________
(vi) Leprosy____________________________________
(vii) Epilepsy____________________________________
(viii) Neurosis____________________________________
(ix) Other serious eg. Asthma______________________
(x) T.B______________________________________

**Other Comments**________________________________________________________________
**Name**______________________________________**Date**__________________**Signature**_____________

**STATION**__________________________________**DESIGNATION**______________________________